HOTUBA YA MHESHIMIWA MKUU WA WILAYA YA ILALA MHE. SOPHIA MJEMA KWENYE KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA WAZEE DUNIANI HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA
1 OKTOBA, 2017

Mganga Mkuu wa Mkoa, Dr.Grace Magembe

Mhe. Naibu Meya wa Manispaa ya Ilala, Omary Kumbilamoto

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala, Ndugu Msongela Nitu Palela

Waheshimiwa Madiwani

Viongozi na Watendaji wa Serikali

Viongozi wa Asasi zisizo kuwa za Kiserikali

Wazee kutoka kata mbalimbali mliopo hapa

Wageni Waalikwa,

Waandishi wa habari,

Mabibi na Mabwana.

Habari za Asubuhi.

Ndugu wananchi,

Awali ya yote napenda kuwashukuru kwa kunialika niwe Mgeni Rasmi katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani. Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa liliamua siku ya tarehe 1 Oktoba ya kila mwaka iwe **Siku ya Kimataifa ya Wazee**. Nia ya Umoja huo ni kutoa nafasi kwa Mataifa kutafakari kuhusu nafasi ya Wazee katika jamii, mahitaji yao, matatizo na ushiriki wao katika maisha yao ya kila siku

katika ujenzi wa taifa la Tanzania. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo kuisherehekea siku hii kwa kutambua mchango wa Wazee kwa Taifa.

Ndugu Wananchi,

Serikali inatambua umuhimu wa wazee katika maendeleo ya Nchi yetu, kwani **Wazee ni rasilimali na hazina** kubwa katika kukuza uchumi wa nchi na kuleta mabadiliko ya kiuchumi. Wazee ndio walinzi wa mali asili tuliyonayo na tunajivunia kwa sasa ,Wazee ndio mliotujengea misingi ya Taifa tuliyonayo hivi sasa. Ndio mlioikomboa Nchi yetu kutoka mikononi mwa Wakoloni, mliochangia kumng'oa Iddi Amini, mliochangia ukombozi wa Nchi za Afrika, mlioweka misingi ya umoja, utaifa na amani tunayotamba nayo leo, mliotunza maliasili tunazofaidi leo, mlioturithisha utamaduni wa Mtanzania, nk. Hivyo, kuwepo kwa Taifa letu ni matokeo na kielelezo tosha cha mchango wenu mkubwa mlioutoa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii.

Kauli mbiu ya mwaka huu

Ndugu Wananchi,

Kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ni **"Kuelekea uchumi wa viwanda , Tuthamini mchango, Uzoefu na ushiriki wa Wazee kwa Maendeleo ya Taifa.** Serikali inalitambua hilo kwa muda mrefu. Kwa mfano, Sera ya Taifa ya Wazee (2003) imeweka bayana kwamba Wazee watashirikishwa katika maamuzi muhimu yanayowahusu wao na yale ya

Taifa kwa ujumla. Sera imeeleza sababu ya kutambua wazee kama rasilimali muhimu katika maendeleo ya taifa letu. Aidha imeanishwa katika sera kuwashirikisha wazee katika uzalishaji mali na hivyo kuondoa umaskini miongoni mwao .Chama cha Mapinduzi (CCM) nacho kinatambua nguvu ya Wazee kwenye maendeleo ya Taifa, Kwa mfano, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015(Kipengele cha 20 (d) ,Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii 2015-2020, Chama Cha Mapinduzi kinaielekeza Serikali kutekeleza na kuhakikisha :- (d) Usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria na miongozo ya ununuzi wa umma, ukaguzi na kusimamia mali za Serikali ili Watanzania wote wanufaike na rasilimali zilizopo pamoja na Sera ya Taifa ya Wazee kwa kuwatumia Wazee ili kuleta maendeleo ya Taifa letu. Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kutekeleza maagizo hayo ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Sera ya Taifa ya Wazee kwa kuwatumia Wazee ili kuleta Maendeleo ya Taifa letu.

Wazee wamekuwa wakitumika kutoa ushauri katika nyanja mbalimbali mfano kwenye Vyama vya Siasa, Mahakama, Bodi za Mashirika na Makampuni, nk. Ushauri huo umekuwa ukitolewa katika ngazi mbalimbali za maamuzi kuanzia Vitongoji na Mitaa hadi Taifa.

Serikali kama ilivyo kwa Wananchi wote inaamini kuwa ushauri wa Wazee ni wa busara unaotokana na uzoefu na ujuzi wa miaka mingi, wametumika kuelimisha vijana kuhusu masuala ya wazee na kuzeeka na kuwajengea uwezo wa kufanya maandalizi ya maisha kuelekea uzee. Hivyo, ushauri wa Wazee ni aghalabu kuwa na makosa na hivyo kuaminika zaidi katika kuleta maendeleo ya Taifa.

Ndugu Wananchi,

Hivi sasa nchi yetu ina wazee takribani milioni 2.4 sawa na asilimia 5.7 ya Watanzania wote. Idadi hii ya wazee inajumuisha waliokuwa wanafanya kazi za kuajiriwa, au waliojiajiri wenyewe na walioko vijijini wakijishughulisha na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Hili ni kundi kubwa ambalo likitumiwa vizuri na hasa kwenye maeneo maalum linaweza kuinua kasi ya maendeleo ya Taifa hili. Ikumbukwe kuwa sehemu kubwa ya kundi hili ina uwezo wa kutumia nguvu ya mwili na akili. Tanzania imetajwa kushika nafasi ya 92 katika orodha ya nchi zenye idadi kubwa ya wazee kati ya nchi 96 duniani kote.

Napenda kusisitiza kuwa Serikali yetu itaendelea kutambua na kuthamini michango inayotolewa na Wazee katika maendeleo ya Taifa letu. Hivyo nawaomba Wazee waendelee kushirikiana na Serikali katika kuchangia maendeleo ya Tanzania.

Wazee na huduma za afya

Moja ya mapendekezo yenu ni la kupewa vitambulisho vitakavyosaidia katika kupata huduma za Afya limetekelezwa kama lilivyoombwa katika maadhimisho yaliyopita . Leo hii Halmashauri ya Manispaa ya Ilala inatekeleza agizo hili sambamba na kuweka bajeti ya dawa katika mpango wa halmashauri .Hii itarahisisha kumtambua mzee na kumrahisishia kupata huduma bila usumbufu wowote.Aidha kuweka

madirisha maalum kwa wazee na kutenga vyumba maalum vya matibabu kuepuka mzee kutumia muda mwingi kwenye foleni.

Utamaduni na Maadili ya Taifa

Ndugu Wazee,

Ningependa pia kuwaomba msaidie katika juhudi za Serikali za kulinda utamaduni wetu na maadili mema ya Watanzania. Utandawazi umekuja na mambo mengi. Mazuri na mabaya. Moja ya mabaya ni kuingiza tamaduni za wenzetu nje ya Nchi na kusahau utamaduni na maadili ya Taifa letu. Mko kwenye nafasi nzuri ya kuona tulikotoka na sasa tuko wapi na kama tuko mahali panapostahili. Ni vema tukakumbushana utamaduni na maadili yatakayotusaidia kuwa na maendeleo.

Mapendekezo ya Wazee

Mhe. Mwenyekiti wa Wazee,

Nakushukuru kwa risala nzuri uliyotoa ikiwa ni salaam ya chama chenu kwa Serikali. Nakiri kuwa maombi na mapendekezo yaliyozungumzwa ni ya msingi, baadhi nimejaribu kuyajibu katika hotuba yangu. Kwa baadhi sina majibu ya papo kwa papo. Yapo mapendekezo ambayo utekelezaji wake ni wa muda mfupi na mengine yatachukua muda kulingana na hali halisi. Mengi ya mapendekezo mliyoyaeleza yametamkwa kwenye Sera ya Taifa ya Wazee (2003). Hata hivyo Mkurugenzi na Mganga Mkuu waliyopewa jukumu la kushughulikia

Wazee wapo hapa. Wamesikia risala yenu natumaini watatengeneza orodha ya hoja zenu na kuweka mkakati wakishirikiana nanyi. Pale maamuzi ya Serikali nzima yatakapohitajika wasisite kuchukua hatua mapema.

Lakini nawiwa kulisemea kidogo hili la vitambulisho vya afya. Ni kweli kuwa kadri umri unavyosogea ndivyo magonjwa nayo yanaongeza kasi ya unyemelezi. Sasa haipendezi kuona kuwa huduma za afya zinakuwa nafuu kwa watu wengine na kuwasahau waliotengeneza mazingira ya unafuu huo.

Ndugu Wananchi,Katika kuhitimisha napenda kuzishukurukwa namna ya pekee Taasisi zote zilizochangia katika kufanikisha kazi ya siku ya leo. Aidha, napenda niwashukuru tena kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi na wote nawatakia maisha marefu na yenye furaha.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.